

## BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1

Fax Nam. + 255 24 2230215

Tovuti: [www.zanzibarassembly.go.tz](http://www.zanzibarassembly.go.tz)



SANDUKU LA BARUA 902,  
ZANZIBAR

Barua Pepe: [zahore@zanlink.com](mailto:zahore@zanlink.com)

### HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA JUU YA TAARIFA YA SERIKALI KUHUSU MAREKEBISHO YA SHERIA YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA ZANZIBAR, NAM. 4 YA 2015

---

**Mheshimiwa Spika**, sina budi kuchukua fursa hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mwingi wa Rehema na Mwenye kurehemu, Muumba wa mbingu na ardhi na vilivyomo kwa kutujaalia uzima na afya njema na kutuwezesha kutekeleza majukumu yetu ya kila siku.

**Mheshimiwa Spika**, pia, ninamshukuru tena Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kuiweka nchi yetu katika hali ya amani, utulivu, umoja na mshikamano mkubwa, hali ambayo imeendelea kuipa nafasi Serikali na wananchi wake kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na mafanikio makubwa. Naomba kuwasisitiza viongozi pamoja na wananchi kwa ujumla, tuendeleo kuidumisha kikamilifu amani na utulivu huo kwani bila ya amani hakuna maendeleo yatakayopatikana.

**Mheshimiwa Spika**, aidha, natumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kwa ajili kutoa maoni ya Kamati yetu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa juu ya Taarifa ya Serikali kuhusu Marekebisho ya Fomu ya tamko la Mali na Madeni chini ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Zanzibar, Nam. 4 ya 2015 ambapo marekebisho hayo yatawezesha kupatikana kwa taarifa zaidi za kiongozi ambazo hazikuwa zinapatikana katika Fomu ya awali.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa hiyo ya Serikali, inapendekeza kufanywa kwa marekebisho katika Jadweli la Pili kwa kulifuta na kuliweka badala yake Jadweli la Pili jipya ambalo linatokana na kifungu cha 41(1) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, nam. 4 ya 2015 (kama ilivyorekebishwa na Sheria nambari 1 ya 2018) ambacho kinampa nguvu na mamlaka Waziri kuweza kufanya marekebisho baada ya kuridhiwa na Baraza la Wawakilishi.

**Mheshimiwa Spika,** naomba sasa kwa ruhusa yako niwataje Wajumbe wanaounda Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kama ifuatavyo:

- |     |                           |                    |
|-----|---------------------------|--------------------|
| 1.  | Mhe. Hassan Khamis Hafidh | Mwenyekiti         |
| 2.  | Mhe. Mtumwa Peza Yussuf   | Makamu Mwenyekiti  |
| 3.  | Mhe. Machano Othman Said  | Mjumbe             |
| 4.  | Mhe. Salma Mussa Bilal    | Mjumbe             |
| 5.  | Mhe. Suleiman Makame Ali  | Mjumbe             |
| 6.  | Mhe. Mohammed Mgaza Jecha | Mjumbe             |
| 7.  | Mhe. Zaina Abdalla Salum  | Mjumbe             |
| 8.  | Ndg. Haji Jecha Salim     | Katibu             |
| 9.  | Ndg. Salma Muhsin Haji    | Katibu             |
| 10. | Ndg. Amina Abeid Hemed    | Msaidizi wa Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** aidha, nachukua nafasi hii kuwapongeza kwa dhati kabisa viongozi na watendaji wote wa Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma, kwa kazi zao nzuri na ngumu wanazozifanya katika kuhakikisha kuwa wanasimamia vyema haki na uadilifu wa viongozi wa Umma Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imeyapitia kwa kina Mapendekezo hayo na haina pingamizi nayo kwa vile yamefuata taratibu zote zinazohusika.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu inawasisitiza viongozi wote wanaohusika, kujaza na kuwasilisha Fomu zao kwa wakati ili lengo la Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Serikali kwa ujumla liweze kufikiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaliomba Baraza lako Tukufu, kuipokea na kuiunga mkono Taarifa hii na inawaomba viongozi wote walioingizwa kwa kupitia Marekebisho haya kuzingatia Sheria.

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Kamati hii Naunga Mkono Hoja.

.....

*(Hassan Khamis Hafidh)*

**Mwenyekiti,**

**Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa,**

**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**